# Fedha kwa ajili ya elimu ya msingi zinakwenda wapi?

**Matokeo Makuu**

- Matumizi ya serikali kwa mwanafunzi mmoja yameongezeka kwa asilimia 70 tangu kuanzishwa kwa elimu ya msingi bure mwaka 2001.
- Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu umekuwa mbaya zaidi tangu 2001; uwiano wa wanafunzi kwa darasa umeendelea kuwa juu sana.
- Bajeti ya elimu ya msingi kwa mwaka inatosha kulipa mishahara ya walimu, vilevile kununua vitabu sita, dawati jipya, na ruzuku ya shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi.
- Haifahamiki vitendea kazi vya elimu vinawezaje kuwa duni kama hali inavyoonesha hivi sasa iwapo serikali inatumia fedha nyingi kiasi hicho.


## Utangulizi

Tangu Serikali ilipoanzisha elimu ya msingi bure mwaka 2001 uandikishwaji wa wanafunci umeongezeka kutoka wanafunzi milioni 4.9 hadi milioni 8.3 katika 2010. Ongezeko la idadi ya wanafunzi limeambatana na ongezeko kubwa katika bajeti ya elimu ya msingi, kutoka Shilingi za Tanzania bilioni 237 katika mwaka wa fedha 2001/02, hadi kufikia karibu mara sita katika kipindi cha miaka 9 baadaye (Shilingi za Tanzania trilioni 1.3 katika mwaka wa fedha 2010/11). Wakati ambapo ongezeko hili la matumizi linawiana na uandikishwaji wa wanafunzi, wastani wa uwiano wa wanafunzi kwa darasa ni 73:1, na uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu wa 51:1 katika mwaka 2010 ni mbaya zaidi kuliko ulivyokuwa katika mwaka 2001 (46:1). Muhtasari huu unahoji ni namma gani bajeti ya elimu ya msingi inavyotumika.

## Jambo la 1: Kuanzia 2001, matumizi kwa mwanafunzi yameongezeka kwa asilimia 70

Tangu kuanzishwa kwa elimu ya msingi bure, bajeti ya elimu ya msingi imepanda mara kadhaa hadi kufikia Shilingi za Tanzania trilioni 1.3 katika mwaka wa fedha 2010/11. Sehemu ya ongezeko hili inatokana na ongezeko kubwa la uandikishwaji wa wanafunzi ; na sehemu nyingine ni kutokana na kupanda kwa gharama za maisha. Inawezekana kudhibiti athari za vipengele hivi tulivyovitaja kwa kukokotoa matumizi kwa bei za mwaka 2010 kwa kila mwanafunzi. Kwa kufanya hivi hali inaonyesha kwamba matumizi halisi kwa kila mwanafunzi yamepanda kwa kiasi cha asilimia 70 tangu 2001. Tunapokokotoa matumizi kwa bei za mwaka 2010 tunaona kwamba kwa sasa serikali inatumia Shilingi 154,000 kwa kila mwanafunzi, ikilinganishwa na Shilingi 94,000 zilizotumiwa katika mwaka 2001.

**Kielelezo 1: Bajeti ya elimu ya msingi kwa kila mwanafunzi kwa bei za mwaka 2010**



## Jambo la 2: Haifahamiki ni jinsi gani bajeti ya elimu ya msingi inatumika

Kwa maelezo mengine, kukiwa na wastani wa wanafunzi 51 kwa kila mwalimu mmoja, inaweza kukadiriwa kuwa serikali inatumia kiasi cha Shilingi milioni 7.8 kwa kila mwalimu kwa mwaka. Kati ya fedha hizi sehemu kubwa inatumika kulipa mishahara ya walimu. Kwa wastani wa Shilingi 300,000 kwa mwezi, au Shilingi milioni 3.6 kwa mwalimu mmoja kwa mwaka, inakadiriwa kuwa serikali inatumia takribani asilimia 46 ya bajeti yake ya elimu katika mishahara ya walimu. Baada ya kuondoa kiasi hicho, kunabaki asilimia 54 ya bajeti au kama kiasi cha Shilingi milioni 4.2 kwa kila mwalimu kwa mwaka kwa ajili ya gharama nyingine. Je fedha hizo zinatumikaje?

**Kielelezo 2: Wanafunzi wengi bado wanakaa sakafuni**



**Picha: Hisani ya Chiku Lweno Aboud**

Ukuzaji mkubwa wa ujenzi ulioambatana na kuanzishwa kwa elimu ya msingi bure sasa umekwisha. Hakuna ushahidi wa kutosha kuonesha kwamba serikali inatumia kiasi kikubwa cha fedha za elimu kugharimia ruzuku ya mwanafunzi (kwa kweli imeonekana kuwa serikali imeshindwa kuigharimia ruzuku kikamilifu), vitabu, au madawati. Iwapo serikali ingetumia kikamilifu fedha zilizotengwa kugharimia vitu hivi, basi upungufu wa vitendea kazi ambao unaziathiri shule nyingi ungeweza kutatuliwa katika kipindi kifupi. Kama inavyooneshwa katika jedwali, baada ya kulipa mishahara ya walimu, kunabaki fedha za kutosha katika bajeti kumpatia kila mwanafunzi kila mwaka dawati jipya, vitabu 6 na shilingi 10,000 ili kufidia gharama za matengenezo ya majengo, vitabu vya walimu, chaki, madaftari, shughuli za utawala, karatasiza  na karatasi za mitihani (*). Pamoja na matumizi hayo bado kungekuwa na fedha zinazobaki kulipia maji, ulinzi, na kadhalika.

**Jedwali 1: Mfano wa namna fedha za elimu kwa mwaka zinavyoweza kutengwa kwa kutumia kigezo cha mwalimu**

| | |
|---|---|
| Bajeti kwa kila mwalimu (wanafunzi 51) | TZS 7,800,000 |
| | minus |
| Makadirio ya mshahara kwa kila mwalimu | TSZ 3,600,000 |
| Vitabu 6 @ TZS 5,000 kwa kitabu @ wanafunzi 51 | TZS 1,530,000 |
| Dawati 1 @ TZS 30,000 kwa kila dawati @ wanafunzi 51 | TZS 1,530,000 |
| Ruzuku @ TZS 10,000 kwa kila mwanafunzi @ wanafunzi 51 | TZS 510,000 |
| | = |
| SALIO | TZS 630,000 |

(*) Kama ilivyo katika sera, ruzuku inapaswa kuwa Dola 10 za kimarekani kwa kila mwanafunzi au kiasi cha Shilingi za Tanzania 15,000 kwa viwango vya kubadilisha fedha mwaka 2010. Ruzuku inajumuisha gharama za vitabu ambazo zimeorodheshwa tofauti.

### Chanzo cha data

Muhtasari huu umetumia data kutoka Takwimu za Msingi za Elimu (Basic Education Statistics) zinazochapishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Data zinaweza kupakuliwa kutoka http://moe.go.tz/statistics.html. Takwimu zinazoonesha kupanda kwa gharama za maisha zimepatikana kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (http://www.nbs.go.tz).

Uwazi
pata picha kamili

Muhtasari huu umeandaliwa na Johannes Hoogeveen wa Uwazi iliyopo Twaweza-Hivos Tanzania.

Uwazi, S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: info@uwazi.org. Tofuti: www.uwazi.org

Umetolewa Machi, 2011.

Twaweza
ni sisi